FUNZO LA 12

1. Shetani alipokuja kumdanganya Hawa, alijificha vipi?
-Ndani ya nyoka.

2. Je, Hawa alijua kuwa ni Shetani aliyekuwa akizungumza na yeye?
-La.

3. Kwa nini Shetani alijificha ndani ya nyoka?
-Kwa sababu Shetani alitaka kumtega Hawa.
-Kwa sababu Shetani alitaka kumdanganya Hawa.
-Kwa sababu Shetani alitaka kumharibu Hawa.

4. Je, hata leo, Shetani hujaribu kuwatega na kuwadanganya watu?
-Ndiyo.

5. Je, hivi leo, Shetani hujaribu vipi kuwatega na kuwadanganya watu?
-Kwanza, Shetani huzungumza na sisi katika mawazo yetu.
-Pili, Shetani huzungumza na sisi kupitia watu wengine.
-Tatu, Shetani huzungumza na sisi kupitia mapepo.

6. Je, Mungu alimwambia Adamu nini kingefanyika kama wangekula kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya?
-Wangekufa.

7. Je, Shetani alimwambia Hawa nini kingefanyika kama wangekula kutoka kwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya?



-Hawangekufa.
-Wangekuwa kama Mungu.

8. Je, Shetani alikuwa anamuita Mungu nini?
-Mdanganyifu.

9. Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, walifanya nini walipotambua kuwa walikuwa uchi?
-Walijifanyia mavazi kutoka kwa majani.

10. Baada ya Adamu na Hawa kutenda Dhambi, walifanya nini walipomsikia Mungu akija kuwaona?
-Walijificha kutoka kwa Mungu.

11. Je, yawezekana kujificha kutoka kwa Mungu?
-La. Mungu yuko kila mahali.

12. Shetani anamchukia nani?
-Shetani anamchukia Mungu na watu wote.

13. Je, Shetani anataka usikilize neno la Mungu?
-La.

14. Kwa nini Shetani hataki usikilize neno la Mungu?
-Kwa sababu Shetani anawachukia watu wote, na anawataka waende katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Ni nini Mungu alichofanya baada ya Adamu na Hawa kutomtii?

Tusome Mwanzo 3:9

9-Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi?

-Baada ya Adamu na Hawa kutomtii Mungu, Mungu alimuita Adamu.

-Je, Mungu alimuita Adamu kwa sababu hakujua alikokuwa Adamu?
-La.

-Mungu anajua kila kitu.
-Mungu anaona kila kitu.

-Hakuna anayeweza kujificha kutoka kwa Mungu.

-Kwa nini Mungu alimuita Adamu?

-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akiri dhambi zake.

-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akubali kuwa hakumtii Mungu.

-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na akubali kuwa alimsikiliza Shetani.

-Kwa nini Mungu anaweza kumuita Adamu?

-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu.



-Kwa sababu Adamu alikuwa wa Mungu.
-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu amtii.

-Kwa nini Mungu anaweza kuwaita watu wote?

-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wote.
-Kwa sababu watu wote ni wa Mungu.
-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wote wamtii.

-Mungu hajabadilika.
-Mungu bado anawaita watu leo.

-Mungu anawaitaje watu leo?

-Kwanza, Mungu anawaita watu kupitia uumbaji wake.

-Uumbaji wa Mungu unaonyesha kuwa kuna Mungu, na kuwa Mungu amefanya kila kitu, na Mungu anataka tumsikilize yeye

-Pili, Mungu huwaita watu kupitia kitabu chake, Biblia.

-Kitabu cha Mungu, Biblia, ni ujumbe wa Mungu kwako.
-Kitabu cha Mungu, Biblia, ni Mungu akiongea na wewe.

-Adamu alisema nini Mungu alipomuita?

Tusome Mwanzo 3:10

10-Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa sababu mimi ni uchi; nikajificha.

-Kwa nini Adamu na Hawa walimwogopa Mungu?
-Kwa sababu hawakuwa wamemtii Mungu.

-Ufuatao ni mfano:

-Kama mwenye shamba atakuja shambani wakati mwizi anaiba mahindi yake, je, mwizi atajificha?
-Ndiyo.

-Kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi na kutomtii Mungu, walijificha kutoka kwa Mungu.

-Mungu alimwambia nini Adamu?

Tusome Mwanzo 3:11

11-Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?

-Kwa nini Mungu alimuuliza Adamu kama amekula lile tunda?

-Je, Mungu alijua kuwa Adamu alikula lile tunda?
-Ndiyo.

-Kwa nini Mungu alimuuliza Adamu kama alikula lile tunda?

-Mungu alimtaka Adamu aje kwake na atubu dhambi zake.

-Mungu alimtaka Adamu amwende yeye na akubali kuwa hakumtii Mungu.



-Mungu alimtaka Adamu amwendee yeye na akubali kuwa alimsikiliza Shetani.

-Kwa nini Mungu anaweza kumuuliza Adamu maswali?
-Kwa sababu ni Mungu aliyemuumba Adamu.

-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wote, Mungu anaweza kuwauliza watu wote maswali.

-Siku moja, Mungu atawauliza watu wote maswali, na watu wote lazima watamjibu.

-Mungu alimuuliza Adamu maswali, na Adamu alijibu vipi?

Tusome Mwanzo 3:12-13

12-Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.
13-Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.

-Adamu alimlaumu Hawa, na Hawa akamlaumu nyoka.

-Mungu tayari alikuwa anajua ukweli.
-Hakuna ukweli uliojificha kutoka kwa Mungu.

-Mtu hufanya nini anaposhikwa akiiba?
-Yeye hujaribu kumlaumu mwingine.

-Tunaweza kuwadanganya wengine kwa kumlaumu mwingine.
-Hatuwezi kumdanganya Mungu kwa kulaumu wengine.

-Mungu anaujua ukweli wakati wote.

-Mungu hua anawaadhibu wale wasiomtii.
-Mungu hua anawaadhibu watenda dhambi.

-Kwanza, Mungu alimwadhibu nyoka.

Tusome Mwanzo 3:14

14-Bwana Mungu akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako;

-Je, Mungu alimwadhibu vipi nyoka?

-Nyoka lazima sasa atambae kwa tumbo lake.

-Kwa nini Mungu aliadhibu nyoka?

-Nyoka hakumwongelesha Hawa.
-Ni Shetani tu aliyemwongelesha Hawa.

-Kwa nini Mungu alimwadhibu nyoka?

-Kwa sababu Mungu huadhibu dhambi zote.
-Kwa sababu Shetani alimtumia nyoka kutenda dhambi.



-Mungu anaadhibu dhambi zote.

-Pili, Mungu alimwadhibu Hawa.

Tusome Mwanzo 3:16

16-Mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.

-Mungu alimwadhibu vipi Hawa?
-Hawa angezaa watoto kwa uchungu mwingi.

-Adhabu ya Hawa ni adhabu kwa wanawake wote.
-Sasa, wanawake wote wanazaa watoto kwa uchungu mwingi.

-Tatu, Mungu alimwadhibu Adamu.

Tusome Mwanzo 3:17-19

17-Akamwambia Adamu, Kwa sababu umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;
18-michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni;
19-kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

-Je, Mungu alimwadhibu vipi Adamu?

-Adamu atalima ardhi kwa jasho jingi, na apate mahindi machache.

-Adhabu ya Adamu ni adhabu kwa wanaume wote.

-Sasa, wanaume wote wanalima ardhi kwa jasho jingi, na wanavuna mahindi machache.

-Mungu alimwadhibu Adamu aje tena?
-Mungu alilaani ardhi yote.

-Ni ishara gani zaonyesha kuwa Mungu amelaani ardhi?

-Kuna miiba na magugu mengi.
-Kuna viangazi vingi na gharika nyingi.
-Kuna mimea na nyoka wengi wenye sumu.

-Wanyama wanawauma wanadamu.
-Watu lazima wafanye kazi sana.

-Watu wanakuwa wagonjwa.
-Watu wanakufa.

-Kwa sababu Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, ardhi imelaaniwa.

-Kwa sababu Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, ardhi imejawa na maovu.



-Kwa sababu Adamu na Hawa hawakumtii Mungu, watu wote wanakufa.

-Adhabu ya kutomtii Mungu ni kifo cha milele.
-Adhabu ya Mungu kwa dhambi ni kifo cha milele.

-Tusome alichosema Mungu alipowaadhibu Adamu na Hawa.

Tusome Mwanzo 3:15

15-nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

-Je, Mungu alikuwa anaongea na nani?
-Mungu alikuwa anaongea na Shetani.

-Mungu alimwambia nini Shetani?

-Mungu alisema kuwa kuna mtu atakayemponda Shetani kichwa, japo Shetani atamuuma kisigino.

-Ni nani atakayemponda Shetani kichwa?
-Mwokozi.

-Muda mfupi baada ya Mungu kuwaadhibu Adamu na Hawa, Mungu aliahidi kufanya nini?

-Muda mfupi baada ya Mungu kuwaadhibu Adamu na Hawa, Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi.

-Mwokozi angefanya nini?

-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za dhambi.

-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za kifo.

-Mwokozi angekuja kuwaokoa watu kutokana na nguvu za Shetani.

-Mwokozi angekuja kupigana dhidi ya Shetani.

-Shetani angemjeruhi mwokozi, lakini Mwokozi angemshinda Shetani.

-Mwokozi angekuwa nani?
-Mwokozi angekuwa mwana wa bikira.

-Kwa nini Mungu aliahidi kutuma Mwokozi?
-Kwa sababu Mungu anawapenda watu wote sana.

-Je, Adamu na Hawa walistahili upendo wa Mungu?
-La.

-Kwa nini Adamu na Hawa hawakustahili upendo wa Mungu?

-Kwa sababu hawakumtii Mungu na walimsikiliza Shetani.

-Kutokutii kwa Adamu na Hawa kulistahili nini?



-Kutokutii kwao kulistahili kifo cha milele.

-Kutokutii kwa Adamu na Hawa kulistahili kifo.
-Lakini Mungu aliahidi kumtuma Mwokozi ili awaokoe.

-Ufuatao ni mfano:

-Mtu mmoja ambaye alikaribia kufa akaja kwako.

-Ukamnunulia dawa na chakula.
-Akaishi na wewe siku nyingi.

-Mwishowe akapona.
-Kabla ya mtu huyo kuondoka, akaiba ng’ombe wako.

-Baadaye, mtu huyo anarudi kwako, akiwa anaelekea kufa.

-Unamnunulia dawa na chakula tena.
-Mtu huyo anapona tena.

-Mtu huyo aliiba ng’ombe wako, anastahili adhabu.
-Lakini, ulimsaidia mtu huyo kupona.

-Kutokutii kwa Adamu na hawa kulistahili kifo.

-Ila Mungu akaahidi kumtuma Mwokozi ili awaokoe.